East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 1, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Matumizi ya Kinaya Kubainishia Maudhui katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Chozi la Heri na Tamthilia ya Kigogo

*Milkah Wanjugu[1*], Prof. Joseph Nyehita Maitaria, PhD[1] na Dkt. Peter Kinyanjui Mwangi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha cha Karatina, S. L. P. 1957-10101 Karatina, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: lwanjugumilkah10@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*08 Juli 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Riwaya, Kinaya, Mtindo, Nadharia ya mtindo na njia ya kimakusudi.*

**IKISIRI**

Mtunzi wa kazi ya kazi ya fasihi hususan riwaya na tamthilia, hutumia mbinu mahususi kuwasilishia matukio na mawazo yanavyoshuhudiwa katika jamii. Mbinu hizo huteuliwa na mtunzi kwa makusudi ili ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa na kueleweka kwa mwafaka na hadhira. Mbinu hizo ni zile zinazojibainisha katika kitengo cha tamathali za usemi. Katika utafiti huu, mbinu inayozingatiwa ni kinaya ambacho huwasilisha ujumbe kinyume na matarajio. Utafiti huu unatuonyesha matumizi ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2017) ambayo imeandikwa na Matei na tamthilia ya *Kigogo* (2015) ambayo imeandikwa na Kea. Wanakejeli uhuru katika mataifa yaliyopata uhuru mwanzoni mwa miaka ya 1960 barani Afrika. Mataifa haya ni yale ambayo baada ya kupigania uhuru na kuunyakua kutoka kwa wakoloni, bado raia wanahisi kuwa wanaendelea kuwa katika hali ya kudhulumiwa na hali ya maisha kuwa magumu kutokana na uongozi usioafiki maono ya matarajio yao. Utafiti huu utabainisha jinsi watunzi wa riwaya na tamthilia teule yaani Assumpta Matei na Pauline Kea mtawalia walivyowasilisha kazi zao kwa kuzingatia mbinu ya kinaya katika kubainishia na kuukejeli uongozi katika bara la Afrika. Malengo ya utafiti huu yatakuwa, kufafanua matumizi ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*, kujadili jinsi waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* wametumia kinaya katika kuendeleza maudhui na kueleza jinsi mbinu ya kinaya ilivyotumiwa katika usawiri wa wahusika viongozi katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya uhakiki wa mtindo na uchanganuzi wa data utaongozwa na mihimili ya nadharia hii kisha matokeo yatawasilishwa kwa njia ya maelezo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

**APA CITATION**

Wanjugu, M., Maitaria, J. N. & Mwangi, P. K. (2023). Matumizi ya Kinaya Kubainishia Maudhui katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Chozi la Heri na Tamthilia ya Kigogo *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 233-242. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303.

**CHICAGO CITATION**

Wanjugu, Milkah, Joseph Nyehita Maitaria and Peter Kinyanjui Mwangi. 2023. "Matumizi ya Kinaya Kubainishia Maudhui katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Chozi la Heri na Tamthilia ya Kigogo". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 233-242. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303.

**HARVARD CITATION**

Wanjugu, M., Maitaria, J. N. & Mwangi, P. K. (2023) "Matumizi ya Kinaya Kubainishia Maudhui katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Chozi la Heri na Tamthilia ya Kigogo", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 233-242. doi: 10.37284/jammk.6.1.1303.

**IEEE CITATION**

M., Wanjugu, J. N., Maitaria & P. K. Mwangi, "Matumizi ya Kinaya Kubainishia Maudhui katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Chozi la Heri na Tamthilia ya Kigogo", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 233-242, Jul. 2023.

**MLA CITATION**

Wanjugu, Milkah, Joseph Nyehita Maitaria & Peter Kinyanjui Mwangi. "Matumizi ya Kinaya Kubainishia Maudhui katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Chozi la Heri na Tamthilia ya Kigogo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Jul. 2023, pp. 233-242, doi:10.37284/jammk.6.1.1303.

## UTANGULIZI

### Usuli wa Mada

Kinaya ni mojawapo ya vipengele vya mtindo wa uandishi. Hutumiwa na watunzi katika riwaya kuonyesha maana iliyo kinyume na matarajio ya watu. Aidha, kinaya huchukua nafasi kubwa sana si tu katika mazungumzo ya kila siku, bali pia jinsi ambavyo mwanadamu anavyotoa mawazo yake. Ni mojawapo ya mbinu zinazotawala maongezi ya mwanadamu hasa kutokana na uwezo wake wa kuficha hisia, maoni na mitazamo yetu sahihi. Kuna aina tofauti za kinaya, kama vile kinaya cha kiusemi, kinaya cha drama na kinaya hali.

Utafiti huu utazingatia dhana ya kinaya kwa jumla vile kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika tamthilia ya *Kigogo* iliyoandikwa na Kea (2015) na *Chozi la Heri* iliyoandikwa na Matei (2017). Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kinaya ni tamathali ya usemi ambayo inahusisha ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa. Aidha ni matumizi ya maneno katika kuelezea hali kwa maana inayokinzana na anachodhamiria msemaji kwa kuyatumia maneno hayo. Matei na Kea wameshughulikia masuala yanayopatikana katika kipindi cha sasa cha uongozi katika maendeleo ya utunzi wa riwaya na tamthilia za Kiswahili.

Masinde (2007) anaeleza kuwa yale yanayoendelea katika jamii humwathiri mtunzi na kumpa tajriba, mguso na ile hamu ya kutunga kwa namna fulani. Zile athari alizopata katika mazingira yake hujitokeza katika tungo zake kupitia mbinu za lugha anazotumia na ujumbe anaowasilisha. Mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumiwa ni kinaya. Aidha, aina za lugha anazotumia mtunzi hutegemea sababu na lengo lake. Kwa misingi hii, utafiti huu ulifanywa kuangazia matumizi ya kinaya katika riwaya na tamthilia teule kwa kuangazia vile Matei na Kea walivyotumia mbinu hii katika kudhihirisha hali duni wnazopitia wananchi, mikononi mwa viongozi waliowateua. Matei na Kea wanawasilisha maudhui mbalimbali kwa kinaya kuwakejeli wananchi barani Afrika ambao, licha ya kudai kuwa huru baada ya wakoloni kuacha kuwatawala, wanaendelea kudhulumiwa na viongozi waliowateua kuwaongoza katika harakati zao za ukombozi na pia kudhihirisha maovu wahusika wengine wanafanyia wenzao jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yao.

### Madhumuni ya Utafiti

- Kufafanua mifano ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*.
- Kujadili jinsi waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

na tamthilia ya *Kigogo* wametumia kinaya katika kuendeleza maudhui mbalimbali.

- Kueleza jinsi mbinu ya kinaya inavyotumiwa katika usawiri wa wahusika viongozi katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*.

**Maswali ya Utafiti**

- Je, kinaya kimejitokeza vipi katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo?*
- Mbinu ya kinaya imetumika vipi katika kuendeleza maudhui kwa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*?
- Wahusika viongozi wamesawiriwa vipi kupitia kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo?*

**Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa wa umuhimu mkubwa katika uwanja wa fasihi kwa kuchunguza kwa mapana na marefu mbinu ya kinaya vile imeendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Pia, kwa wasomi utawapa mwelekeo na uelewa jinsi ya kuchanganua kinaya kitaaluma. Zaidi ya hayo, utafiti huu utakuwa dira na mwongozo kwa watafiti wa baadaye watakaochunguza zaidi kuhusu mbinu ya kinaya katika riwaya na tamthilia teule.

Utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya fasihi na utunzi wa riwaya na tamthilia za Kiswahili. Kwanza, unatoa mchango wa kubainisha usawiri wa mbinu ya kinaya na aina zake katika riwaya na tamthilia za Kiswahili. Pili, utafiti huu umeweza kujadili jinsi waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* wametumia kinaya katika kuendeleza maudhui katika kazi zao. Tatu, utafiti huu unachangia kuonyesha vile wahusika wamesawiriwa kupitia mbinu ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya. *Kigogo*

**NADHARIA YA UTAFITI**

Nadharia ambayo imeongoza utafiti huu ni ile ya uhakiki wa kimtindo ambayo imeonyesha jinsi kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Miongoni mwa waasisi muhimu wa nadharia hii ni Coombes (1953) anayeeleza kuwa, ili kuchanganua fasihi kwa undani hatuna budi kuzingatia matumizi ya lugha. Coombes anasema kwamba, ili kuchanganua mtindo katika kazi fulani, lazima vipengele vinavyofanya kazi hiyo vivutie ili vizingatiwe. Anaendelea kuzungumzia vigezo kama vile matumizi ya taswira, wazo la kishairi, hisia zinazoibuliwa, uteuzi wa maneno, urari wa vina na mahadhi ya shairi.

Leech na Short (2007) wanaendeleza nadharia hii ya kimtindo pale wanaposisitiza kuwa nadharia hii ya kimtindo inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Wanaendelea kusema kuwa uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo na husaidia katika uelewekaji wa matini ya kazi ya fasihi. Maelezo haya yamefaa sana utafiti huu kwa kuwa, nadharia hii ya mtindo imedhihirisha vile Matei na Kea wametumia kinaya katika kuonyesha vile viongozi wanadhulumu raia wanaowaongoza hata baada ya kupata uhuru miaka hamsini iliyopita.

Wamitila (2008) anaendeleza nadharia hii ya kimtindo pale anaposisitiza kwamba, nadharia hii inadhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi. Kimsingi, anaashiria kuwa uhakiki wa mtindo huhusu kuchanganua vipengele vya fasihi na pia vya isimu. Hii inamaanisha kuwa tunapohakiki mtindo katika fasihi, hatuwezi kupuuza matumizi ya vipengele vya kiisimu pia kwa kuwa hutumiwa kuonyesha sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi.

Nadharia hii itaongozwa na mihimili kama vile: Kwanza uhakiki wa mtindo hujihusisha na uchunguzi wa kinachosemwa ambacho ni ujumbe na kinavyosemwa ambacho ni mtindo. Mhimili huu utafaa utafiti huu kwa kuwa, utaonyesha jinsi kinaya

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

kinadhihirisha ujumbe wa waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* yaani Matei na Kea. Pia utaonyesha vile kinaya huendeleza maudhui katika riwaya hizi na jinsi viongozi wamesawiriwa katika kutenda matendo ambayo ni kinyume cha matarajio ya watu.

Pili, nadharia ya uhakiki wa kimtindo pia husisitiza kuwa, kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao unapochanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji wa undani wa matini za fasihi kulingana na madai ya Simpson (2004). Mhimili huu utaufaa utafiti huu kwa kuwa utaonyesha vile waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* walivyotumia ubunifu katika kazi zao. Kwa mfano walitumia kinaya katika kuwasilisha maudhui potovu yaliyoibuliwa na wahusika waliokuwa wanadhaniwa kuwa wenye hulka nzuri lakini wakatenda mambo ambayo ni kinyume cha matarajio ya jamii.

Tatu, fasihi haiwezi kujadiliwa bila kuzingatia kuwa ina matumizi maalum ya lugha kulingana na Chapman (2012). Haya maoni yanaungwa mkono na Turner (1984) anaposema kwamba uteuzi wa maneno si huru na msanii hulazimika kuwa makini ili kazi yake ikubalike na walengwa au hadhira yake. Maelezo haya yanafaa utafiti huu kwa kuwa utaonyesha vile waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* walivyotumia umahiri wao katika uteuzi wa lugha katika kazi zao. Kwa mfano kwa sababu hawakuwa wanataka kudhihirisha maovu ya viongozi moja kwa moja, waliteua kinaya kinachotumika kama kioo kwa jamii kuona na kuelewa mambo yanayotendwa na viongozi hawa yaliyo kinyume cha matarajio yao.

Nne, lugha ndicho kigezo muhimu cha kupimia ufanisi wa kazi ya fasihi kulingana na Ngara (2011). Kazi ya fasihi huwa na sehemu kama dhamira, maudhui na wahusika. Lakini bila lugha, vipengele hivi haviwezi kuwasilishwa vilivyo, sehemu hizi hupewa umbo kupitia kwa lugha. Maelezo haya yamefaa utafiti huu kwa kuwa yataonyesha vile kinaya kimewasawiri viongozi katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* kwa kuainisha maudhui na kutekeleza dhamira ya waandishi Matei na Kea.

## MBINU ZA UTAFITI

### Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kiuthamano, ulitumia mbinu ya usomaji makini na uchunguzi wa riwaya na tamthilia teule yaani: riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kuzihakiki riwaya na tamthilia teule kwa kutumia na kuongozwa na msingi wa nadharia ya uhakiki wa kimtindo.

### Uteuzi wa Sampuli

Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi fulani cha vitu au watu kilichomo ndani ya mkusanyiko wa watu ambacho mtafiti anaamini kwamba kikundi hicho kitampatia taarifa anayohitaji kuhusu utafiti wake. Kwa sababu hiyo, mtafiti hulazimika kuteua kitu fulani au watu ambao huitwa kundi lengwa. Kwa hiyo katika utafiti huu, mtafiti alitumia riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* kwa sababu riwaya na tamthilia hizi zimesheheni mbinu ya kinaya ambayo mtafiti alikusudia kukichunguza kwa kina kwa kuangazia mifano ya kinaya, jinsi kinaya kimetumika katika kubainisha maudhui mbalimbali na jinsi wahusika wamesawiriwa katika riwaya na tamthilia teule.

### Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Pandey na Pandey (2021) wanasema kwamba zipo mbinu mbalimbali za kukusanya data na katika mbinu hizo hakuna mbinu inayojitosheleza katika mazingira yake. Mbinu ya usomaji matini kwa kusoma vitabu teule, riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* ilitumiwa. Data ilikusanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Tasnifu zenye uhusiano na mada ya mtafiti pia zilisomwa kwa makini.

#### *Mbinu ya Maktaba*

Kothari (2004) anaelezea mbinu hii kuwa ni mbinu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, tahakiki, magazeti, majarida na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti ili kupata data zilizokidhi haja ya kiutafiti pamoja na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Data zilizokusanywa kutoka riwaya na tamthilia teule ziliteuliwa na kupangwa ili zichambuliwe kwa urahisi. Uchunguzi huu wa kina uliwezesha mtafiti kuhakiki kwa makini kinaya kilivyotumika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* na jinsi kinavyosaidia kuwasawiri wahusika kama wenye hulka hasi.

### Vifaa vya Ukusanyaji wa Data

TUKI (2006) wanafasili data kuwa ni taarifa au takwimu ambayo hutumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja fulani. Vifaa vya kukusanyia data ni vifaa mbalimbali ambavyo hutumika katika kukusanya na kuhifadhi data za utafiti. Katika harakati za kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alitumia vifaa mbalimbali kama; Shajara na kompyuta mpakato.

#### *Kompyuta Mpakato*

Kompyuta ni mashine ya kielektroniki ya kuhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa, kukokotolea na kuongoza mitambo. Pia, kwa upande wa kompyuta pakatwa, hii ni aina ya kompyuta inayoweza kubebeka kwa urahisi kutoka sehemu moja hadi nyingine ambayo huweza kupakatwa. Katika utafiti huu, kompyuta pakatwa ilimsaidia mtafiti wakati wa kuandaa pendekezo la utafiti, kuhifadhi data zilizokusanywa, na kuandika ripoti ya utafiti. Aidha, kalamu na karatasi ni vifaa vya asili katika ukusanyaji wa data ya utafiti. Bila shaka vifaa hivi vitaendelea kutumika kwa miaka mingi ijayo. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia daftari na kalamu ambavyo vilimsaidia katika kuhifadhi kumbukumbu za uchanganuzi wa kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

### Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Ali na Peterson (2014) uchambuzi wa data ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma kazi ya fasihi kwa lengo la kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo na kadhalika. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itaasaidia kujibu maswali ya utafiti unaohusika. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo katika kuchanganua data za utafiti kwa kuwa data za utafiti huu zilikusanywa kwa mkabala usio wa kiidadi, pia uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kiuthamo. Kutokana na hali hiyo data zilikusanywa kutoka riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* ziliwekwa katika makundi na kisha kuwasilishwa ili kuweza kufikia malengo mahususi ya utafiti huu.

## UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

### Riwaya ya *Chozi la Heri*

Riwaya ya *Chozi la Heri* iliandikwa na Assumpta K. Matei mwaka 2017. Riwaya hii imejikita katika kinaya. Imeakisi vile wahusika wanateseka na kulia machozi ya uchungu ambayo ni kinyume cha anwani ya riwaya hii ambayo inataja kuwa machozi ni ya furaha. Ina sura kumi kwa utaratibu ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kukosoa jamii iliyokwamia katika ukabila na uhifadhina pale ambapo raia wanachagua viongozi kwa kuwa ni wa jamii yao na pia kuwa na ubaguzi kwa wanawake kwa kushikilia kuwa wanaume ndio wanafaa kuongoza jamii lakini sio wanawake. Kinaya kinajitokeza pale viongozi hao wanaume wanawatendea maovu jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yao.

### Tamthilia ya *Kigogo*

Tamthilia ya *Kigogo* iliandikwa na Pauline Kea mwaka wa 2016. Tamthilia hii imejikita katika kinaya. Imeakisi vile viongozi wanavyowadhulumu raia waliowachagua jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yao. Tamthilia hii imeakisi mandhari ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

usasa ambapo ina maonyesho saba yaliyopangiliwa vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kudhihirisha vile viongozi wanavyojilimbikizia mali na kuwasahau wananchi waliowachagua na vile wanawadhulumu kama vile kuwafunga jela bila makosa yoyote.

**Aina za Vinaya Katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo***

Sehemu hii inajadili na kufafanua lengo mahususi la kwanza ambalo lilitaka kuchunguza mifano ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* kama ifuatavyo:

***Kinaya cha Hali***

Hiki ni kinaya kinachodhihirisha hali iliyo kinyume cha matarajio ya watu. Kwa mfano katika riwaya ya *Chozi la Heri* kuna hali ya uzinzi kama vile kitendo cha bwana Tenge kufanya vitendo vya ufuska na wanawake wengine tena ndani ya nyumba yake na mbele ya macho ya watoto wakati mkewe alikuwa mbali na nyumbani. Pia kitendo cha mwalimu Fumba kushiriki mapenzi na mwanafunzi wake Rehema ilhali mwanafunzi huyo alikuwa katika kidato cha tatu (Uk. 103). Katika tamthilia ya *Kigogo*, kuna hali ya unafiki pale tunamwona Majoka akikiri kuwa ana moyo wa huruma ilhali anafanya vitendo vya kikatili (Uk. 34). Kwa mfano, Majoka hamhurumii Ashua wakati Ashua anapoenda kuomba msaada kwake. Anataka kufanya ngono naye kwanza na anaishia kumtupa korokoroni bila makosa yoyote.

***Kinaya cha Mazungumzo***

Kinaya hiki hutokea pale ambapo mzungumzaji huzungumza jambo ambalo ni kinyume na matendo yake. Mfano katika tamthilia ya *Kigogo*, tunapata Kenga akisema kuwa wafadhili kutoka mashariki na magharibi wametoa pesa za kufadhili mradi wa kuchonga kinyago cha Marara bin Ngao. Hiki ni kinaya kwa kuwa kina Tunu wanapofadhiliwa ili wapate rasilimali za kupinga utawala wa kiimla, kina Majoka wanadai kuwa hao wafadhili wafukuzwe kwa sababu wanajiweza wenyewe kwa wenyewe huko Sagamoyo (Uk. 11). Kinaya hiki kinadhihirisha unafiki wa Kenga pale anasema kuwa wafadhili wanawasaidia kwa pesa kwa hivyo hatungetarajia Majoka kusema hao wafadhili wafukuzwe. Pia katika riwaya ya *Chozi la Heri,* ni kinaya kwa Lunga Kiriri Kangata aliyekuwa mstari wa mbele kudumisha misitu na kupigia debe utunzaji wa mazingira anapogeuka. Baada ya kufutwa kazi, anaenda msitu wa Mamba na kuangusha miti na kufungua mashamba makubwa. Ni kinaya mamake Sauna kumwambia mwanawe asimpake tope baba aliyembaka badala ya kumkemea baba huyo na kumchukulia hatua za kisheria (Uk. 155).

***Kinaya cha Drama***

Hiki ni kinaya kinachoonyesha wahusika wakiigiza lakini kinaya ni kwamba huwa hawatendi yale wanaigiza bali hufanya kinyume cha matarajio yao. Mfano ni katika *Chozi la Heri* pale tunapata Mwangeka, Tila na marafiki wao wakiigiza kuhusu kifo cha ndugu yao Dede aliyekufa akiwa na miaka sita. Walitia boksi mwanasesere wakampa jina la Dede, wakajilazimisha kupiga ukemi na machozi ya dhati yakatwaa nafasi ya mate (Uk. 60). Ni kinaya kwa kuwa walikuwa wanaigiza kama ni mazishi lakini huu ulikuwa tu mchezo wa watoto. Mfano mwingine ni katika tamthilia ya *Kigogo* pale tunapata mhusika Majoka akiigiza sauti ya Ashua kwa kusema, “La, koma, siwezi mimi”. “Sitaki kuwa gurudumu la akiba”(Uk. 19). Ni kinaya kwa kuwa Majoka alikuwa anaomba Ashua ajihusishe naye kimapenzi na kuigiza kwake hakuwa anamaanisha Ashua asiwe mpenzi wake kwa kuwa alikuwa mzinzi.

***Kinaya katika Kubainisha Maudhui ya Ufisadi***

Sehemu hii inajdili na kufafanua lengo mahususi la pili mbalo liliuliza vile kinaya kimetumika katika kubainisha maudhui mbali mbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Kwa mujibu wa utafiti huu, inaonekana kuwa katika jamii zinazoakisiwa na waandishi, kinaya kimetumika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

kuendeleza maudhui ambayo ni kinyume cha matarajio ya watu. Kwa kutumia mbinu ya maktaba, yaani usomaji na uchambuzi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* na tafiti za awali, utafiti huu ulichunguza vile mbinu ya kinaya inatumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya na tamthilia teule. Uchanganuzi wa kinaya umeongozwa na nadharia ya uhakiki wa kimtindo ambayo mtafiti ameiteua kuitumia katika utafiti huu. Hivyo basi, uchanganuzi na usomaji wa kazi za kifasihi zilizotambuliwa hapo juu, mtafiti amepata vile mbinu ya kinaya imetumika katika kuendeleza maudhui kama ifuatavyo:

Kuna ufisadi katika wizi wa mali ya umma ,mfano Katika *Chozi la Heri* kuna watu waliojenga majumba yao katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya barabara na wengine wakajenga chini ya vigingi vya nyaya za umeme. Baada ya serikali kuwapa ilani ya kuondoa majumba yao, kuna baadhi ya mabwanyenye hawa walionekana wakitoa milungula hadharani (Uk. 13). Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo tungetarajia hawa mabwanyenye kuchukuliwa hatua na serikali lakini wanatoa hongo ili na kuendelea kumiliki maeneo haya. Ufisadi mwingine unajidhihirisha wakati mashamba madogomadogo ya wananchi yaliponyakuliwa na mabwanyenye ambao walikuwa na maelfu na maelfu ya ekari ambapo walijenga viwanda na maduka ya biashara huku wengine wakilima mashamba makubwa anajidhihirisha wakidai kuwa ni njia ya kuhakikishia wenyeji wanajitosheleza kwa chakula. Wananchi wanapolalamika kuhusu kashfa hii ya unyakuzi kinaya ni kwamba, huambiwa kuwa tume ya kuchunguza unyakuzi imeundwa. Cha kushangaza ni kwamba wananchi hawazioni ripoti zitokanazo na kashfa hizo (Uk. 22). Ufisadi pia unajitokeza katika hospitali za umma pale kuna wizi wa dawa zilizotengwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa. Ufisadi huu unamkera Selume ambaye ni muuguzi katika hospitali hiyo kwani wagonjwa wanakosa huduma za msingi kwa sababu shehena za dawa zilizotengewa hospitali ya umma zinaishia kwa maduka ya dawa ya wasimamizi wa hospitali.

Katika tamthilia ya *Kigogo* kinaya cha ufisadi kinajitokeza pale wafanyabiashara hutozwa kodi ya kiwango cha juu kupita kiasi. Hata baada ya wao kutozwa kodi ya kiasi hicho, soko lao halisafishwi. Hatimaye, linafungwa kwa kisingizio kwamba lina uchafu unaoliharibia Jimbo la Sagamoyo sifa. Ukweli wa mambo ni kuwa pesa za kulisafisha soko zimefujwa jinsi inavyobainika wakati Kenga anapoeleza madai ya Tunu kwa vyombo vya habari (Uk. 32). Pia ni kinaya kwa Majoka kuwaruhusu wafuasi wake kuvunja sheria. Asiya amepewa kibali cha kuuza pombe haramu ingawa kufanya hivyo ni kinyume na sheria. Hali hii ya kutofuata sheria imekikithiri jimboni hadi ikawavimbisha baadhi ya watawaliwa kichwa kiasi cha kujipiga kifua wakisema kwamba katiba na serikali ni mambo mawili tofauti, Yaani mtu halazimiki kufuata sheria mradi yuko upande wa serikali. Mbali na hayo, wafuasi wa Majoka wameruhusiwa kukata miti ovyoovyo na kuiuza kwa manufaa yao ya kibinafsi. Majoka hajali madhara ya uharibifu wa mazingira. Labda biashara hii ya miti inamnufaisha kwa njia fiche (Uk. 53).

***Kinaya katika Kubainisha Maudhui ya Unafiki***

Unafiki ni hali ya mtu kujifanya mwema kwa lengo la kuyaficha maovu. Kinaya kinatumika kuendeleza maudhui haya kwa kuwa kuna wahusika katika riwaya na tamthilia teule wanaojifanya wema mbele za watu lakini inadhihirika kwamba wanatenda maovu kinyume na matarajio ya watu kama vile:

Viongozi kutumia udanganyifu kuwashawishi watu wawachague katika uchaguzi. Mfano ni kutoka riwaya ya *Chozi la Heri* pale ambapo viongozi wanatumia ahadi hewa kwa vijana kwamba wakiwateua watawaajiri kazi lakini baada ya kuchaguliwa hao viongozi wanawasahau. Hili linadhihirika pale tunamwona kijana Dengelua akitamauka na kuwa mlevi kupindukia na kupita kwa mtaa wa Tononokeni akiimba usiku na kuelezea vile amesoma hadi chuo kikuu lakini akakosa kazi (Uk. 133).

Katika tamthilia ya *Kigogo* viongozi wanatumia

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

udanganyifu kwamba wataongeza mishahara ya walimu na wauguzi kisha wapandishe kodi ndipo pesa hizo ziwarejee. Kenga naye anasema kuwa hiyo ni mbinu ya kutia kwa kushoto na kutoa kwa kulia. Huu ni unafiki kwa kuwa watawala wanahakikisha kuwa wanapata sifa nzuri kwa kuongeza mshahara na wakati uo huo watumishi wa umma wanazidi kuwa maskini kwa kuongezewa kodi ili wawe mbioni kujitafutia riziki na wasiyatilie maanani maovu yanayotendeka (Uk. 36).

### *Kinaya katika Kubainisha Maudhui ya Ukatili*

Ukatili ni kuwatendea watu matendo ya kinyama kwa kukosa huruma. Mfano ni katika riwaya ya *Chozi la Heri* pale wafuasi wa mpinzani wa Mwekevu anayeitwa Mwanzi wanawatendea ukatili wafuasi wa mgombea mwenza Mwekevu. Mfano tunamwona kijana aliyekuwa na shati lililoandikwa Hitman akichoma magari ya wenyewe (Uk. 24). Pia tunawaona watoto wa kike wa Kaizari ambao ni Lime na Mwanaheri wanapobakwa na wafuasi wa mpinzani wa Mwekevu, tena mbele ya macho ya baba yao (Uk. 25).

### Kinaya katika ***Kubainisha Maudhui ya Uongozi Mbaya***

Uongozi mbaya ni pale viongozi hawatekelezi wajibu wao kama vile inavyofaa. Kuna kinaya katika uongozi mbaya pale ambapo viongozi wanafanya kazi kinyume cha matarajio ya watu katika riwaya na tamthilia teule. Mfano katika riwaya ya *Chozi la Heri*, uongozi mbaya unadhihirika pale ambapo nchi ya uhafidhina bado inategemea mataifa yaliyoendelea. Uchimbaji wa raslimali zilizopo unafanywa na makampuni ya nje. Raia wanaajiriwa kwa mishahara duni kabisa. Shamsi na wenzake walijaribu kuandamana wakafutwa kazi (Uk. 133). Katika riwaya hii pia kuna ukiukaji wa haki za kibinadamu. Kwa mfano waandamanaji waliofunga barabara na kukataa kubanduka walipigwa risasi na kuuawa.

Katika tamthilia ya *Kigogo*, uongozi mbaya umejitokeza kwa njia mbalimbali kama vile, kuwepo kwa tengatawala pale ambapo katika jimbo la Sagamoyo kuna sumu ya nyoka; Yaani uhasama unaopandwa na viongozi ili kugawanya wananchi. Kwa mfano, Sudi ana uhasama na Boza ambaye ni mchonga vinyago mwenzake. Sababu ya uhasama wao ni kwamba watu hao wako katika mirengo tofauti ya kisiasa. Aidha, Ngurumo na kundi lake la walevi tayari wameshatiwa sumu na utawala wa Majoka, hivyo wanawahasimu wanaharakati Tunu na Sudi. Uongozi mbaya pia unadhihirika pale Majoka anatumia madaraka yake kujilimbikizia mali. Anamiliki *Majoka and Majoka Company*, *Majoka and Majoka Modern Resort* pamoja na *Majoka and Majoka Academy*. Vile vile bado anakwapua eneo la soko ili ajenge hoteli yake ya kifahari. Aidha, Mamapima anatoa hongo ya uroda kwa Ngurumo ili apate mradi wa kuoka keki ya uhuru (Uk. 64).

### Jinsi Kinaya Kimetumika katika Kusawiri Sifa za Wahusika

Sehemu hii inajadili na kufafanua lengo mahususi la tatu ambalo lilitaka kuchunguza vile kinaya kinatumika katika kujenga sifa za wahusika. Kwa mujibu wa utafiti huu, inaonekana kuwa katika jamii zinazoakisiwa na waandishi, kuna wahusika wanaotenda maovu jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya watu. Kwa mfano katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunapata mhusika Sauna ambaye alijifanya mzuri sana kwa waajiri wake, kama vile Lunga Kiriri Kangata na anaaminiwa sana na hao waajiri wake lakini mwishowe anawatorosha watoto wao kama vile Dick na Mwaliko na kwenda kuwauza (Uk. 84).

Katika tamthilia ya *Kigogo* unampata mhusika Majoka ambaye ni kiongozi wa Sagamoyo. Tungetarajia awe na hulka nzuri lakini anatenda maovu jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yetu. Kwa mfano tunapata kuwa yeye ni muuaji pale anawaua watu ovyoovyo, kinyume na sheria .Katika maungamo yake akipelekwa hospitalini, nafsi yake inamsuta kutokana na mauaji aliyotenda; anasema kwamba damu inamlilia. Hii inamaanisha kuwa ameshiriki katika mauaji ya watu wengi kama Jabali aliyekuwa mpinzani wake aliyekuwa na chama cha

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Mwenge. Pia, Majoka na Kenga wanapanga kumuua Chopi kwa kuwa aliteleza katika majukumu yake, na anafahamu njama zao na wanahofia huenda akazifichua (Uk. 68). Tena, Tunu anamwambia Majoka, "Nyinyi ni wauaji" (Uk. 43).

**HITIMISHO**

Utafiti huu ulichunguza kinaya katika riwaya na tamthilia za Kiswahili ambazo ni riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Lengo kuu ni kuangazia usawiri wa Kinaya vile waandishi wa kazi hizi za kifasihi wanavyosawiri mbinu ya kinaya katika kuelezea matukio katika jamii kwa riwaya na tamthilia teule, tafiti zilizotangulia zilijikwepa. Katika riwaya na tamthilia hizi, waandishi wanadhihirisha vile wahusika wanavyofanya maovu jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya jamii. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, mwandishi anamuonyesha mhusika Mwalimu Fumba anayefanya uzinzi na mwanafunzi wake Rehema jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya taaluma yake na pia kwa jamii. Vilevile, katika tamthilia ya *Kigogo*, mwandishi anamuonyesha mhusika Majoka kiongozi wa Sagamoyo ambaye anafanya uzinzi na wanawake nje ya ndoa yake. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*, waandishi hawakufafanua kwa kina athari zilizowapata wahusika waovu kwa kujihusisha na uovu. Ukosefu wa kufafanua kwa kina mbinu ya kinaya na athari zote zilizomo, huacha pengo la kutowapa wasomaji mafunzo kamili kuhusu suala la uzinzi maana kwamba wasomaji hawatapata faida hasi na chanya kuhusu uovu.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulichunguza mbinu ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Kwa hakika, hakuna utafiti ambao unaweza kuchukuliwa kuwa umekamilisha suala husika katika mada ya utafiti. Hivyo basi, ni wazi kwamba utafiti huu haukudadavuliwa na kutosheleza mbinu ya kinaya katika utanzu wa riwaya na tamthilia ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti zaidi unahitajika kuchunguza kinaya katika kazi nyingine za fasihi kama vile; Ngano, mashairi, hadithi fupi na nyimbo. Hali kadhalika utafiti wa ziada unaweza kufanywa kuhusu mbinu ya kinaya katika kazi ya fasihi yoyote na vile kinatumika katika kubainishia maudhui.

**MAREJELEO**


Ali, N. B., & Petersen, K. (2014, September). Evaluating strategies for study selection in systematic literature studies. In *Proceedings of the 8th ACM/IEEE international symposium on empirical software engineering and measurement* (pp. 1-4).

Augustine, M. (1990). *Usawiri wa wahusika makahaba katika Riwaya za Said Ahmed Mohammed*. Tasnifu Ya uzamili Chuo kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Chapman, R. (2012). *The languge of English Literature London*: Edward Arnold Publishers Ltd.

Coombes, J. (953). *Literature and criticism*. London: Penguin Books Middlesex.

Cuddon, John A. (1999). *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theories*. Revised by C. Preston. London: Penguin.

Kea, P. (2016). *Kigogo*. No boundaries Ltd.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques*. New Age International.

Lakoff, G., & Johnson, M. (1980*). Metaphors we live by*. University of Chicago, Chicago, IL.

Leech, G. N., & Short, M. (2007). *Style in fiction: A linguistic introduction to English fictional prose* (No. 13). Pearson Education.

Magaju, J. K. (2004).*Uhalisia ajabu katika Riwaya ya Said A. Mohammed, Babu Alipofufuka (2001) na Ya Wamitila, Bina-Adamu (2002).* Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Masinde, E. (2007). *Ufundishaji wa ushairi katika shule upili na vyuo*. Nairobi. Taaluma Publishers.

Matei, A. K. (2017). *Chozi la Heri*. One planet publishing & Media services Limited.

Musee, D. (2007). *Matumizi ya Majazi kama Mkakati wa Kuepuka Upigaji Marufuku katika Riwaya za Mkangi*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Ngara, E. (2011). *Stylistic Critism of the African Novel*. London: Nairobi: Heineman.

Pandey, P., & Pandey, M. M. (2021). *Research methodology tools and techniques*. Bridge Center.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for students*. London : Routldege.

Tuki (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Turner, G. W. (1984*). Stylistics.* Harmond Sworth: Penguine.

Wamitila, K. W. (2008). *Kazi ya fasihi : Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi : Vide-Muwa Publishers Ltd.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.